KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 14, Issue 2

11th Shawwâl 1432

9th Sept, 2011

YALIYOMO

MAUTI 1 - 3

UMUHIMU WA SUNNAH 3 - 4

MAFUNZO YA KIHAKIKA YANAYOTOKAMANA NA MAUTI

Na: Sheikh Muhammad al-Jibaaly

NI LADHA AMBAYO KILA MWANA-ADAMU ATAIONJA

Mauti ni matukio ya yakini. Kila mwana-adamu atakumbana nayo na ataonja uchungu wake. Kila muda wa maisha ukipita, basi unatukurubisha na mauti yetu yasiyokuwa na shaka.

Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"Kila nafsi itaonja mauti. Na bila shaka mtapewa ujira wenu kamili siku ya Kiyama. Na aliyewekwa mbali na moto na akaingizwa Peponi, basi amefuzu (amefaulu kweli kweli). Na maisha ya dunia (hii) si kitu ila ni starehe idanganyayo (watu).** [Aali 'Imraan 3:185]

Hakuna mwana-adamu yoyote atakae au aliye-epushwa na machungu ya mauti - hata Mitume na Manabii.

Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Nasi hatukumfanya mwana-adamu yoyote wa kabla yako aishi milele. Basi kama ukifa wewe wao wataishi milele? Kila nafsi itaonja mauti, na tunakufanyieni mitihani kwa (mambo ya) shari na ya kheri; na kwetu (nyote) mtarejeshwa."** [Al-Anbiyaa' 21: 34-35]

Imepokewa kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها) yakwamba katika maradhi yake ya mwisho, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa karibu naye chombo cha (birika la) maji; alikuwa akitia mkono wake ndani ya maji hayo, na akijipangusa uso wake huku akisema: *"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah. Kwa hakika mauti yana hali ya mvinyo!"* Baada ya kuyarudia rudia maneno hayo kwa mara kadhaa, alinyosha mkono wake na akasema: *"Yaa Allaah! Nakuomba msamaha, na unirehemu, na unija'aliye nijiunge pamoja na rafiki yangu wa juu zaidi."* Kisha baada ya hapo Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaaga dunia na mkono wake ukalegea na kuanguka [al-Bukhari].

Machungu ya mauti huchukuwa muda mrefu kushuka, hata kwa mtu ambaye ni mcha Mungu. Amepokea Jaabir Bin Abdillaah yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Kuweni huru katika kusimuliana kuhusu matukio kutoka kwa wana wa Israa'eel, kwa sababu mambo ya kushangaza yaliwahi kuwatokezea wao."* Kisha akasimulia: "Kundi la watu miongoni mwa wana wa Israa'eel walikwenda katika sehemu fulani ya makaburi yao. Wakasema (kuambiana wao kwa wao), 'Hebu tuswalini raka'ah mbili, kisha tumuombe Allaah (عزّ وجلّ) atufufulie mtu miongoni mwa waliokufa ili tumuulize kuhusu mauti.' Wakafanya hivyo, na baada ya muda mchache, mtu mmoja akainua kichwa chake kutoka katika kaburi mojawapo. Alikuwa ni wa rangi ya kahawiya, na alama ya sijda baina ya macho yake mawili. Akasema, 'Enyi watu! Mwataka nini kutoka kwangu mimi? Tangu nilipokufa mpaka sasa ni muda wa miaka mia moja, na joto la mauti halijawacha kuniondokea mpaka hivi punde tu. Niombeeni kwa Allaah (عزّ وجلّ) Anirudishe katika hali yangu (ya mauti) niliyokuwa hapo awali.'"

HAPANA CHA MAFICHO KUTOKANA NA MAUTI

Ufikapo muda tuliokadiriwa, mauti ni yenye kutufika bila ya kujali mahala tulipo. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Po pote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome madhubuti."** [An-Nisaa' 4:78].

Hata kama tukijaribu kuyakimbia mauti, tutakumbana nayo. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **Sema: "Hakika mauti haya mnayoyakimbia, bila shaka yatakutana nanyi; kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri; hapo atakujulisheni (yote) mliyokuwa mkiyatenda."** [Al-Jumu'ah 62:8].

Katika muda tuliopangiwa ambao Allaah (سبحانه وتعالى) aliouweka kwa mauti yetu, hapana awezae kuzizuiya roho zetu zisitoke kwenye miili yetu: Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Basi mbona (roho) ifikapo kooni na nyinyi wakati ule mnatazama. Nasi tunakaribiana naye zaidi (huyo anayetoka roho) kuliko nyinyi, wala nyinyi hamuoni. Kama nyinyi hamumo katika mamlaka (yangu). Kwa nini hamuirudishi (hiyo roho), ikiwa mnasema kweli (kuwa hamumo katika mamlaka yangu).?"** [Al-Waaqi'ah 56:83-87].

KUJITAYARISHA KWA MWISHO

- KUSHUGHULIKA NA MAMBO YA KIDUNIA.

Jee, tuko tayari kwa hiyo siku isiyokuwa na shaka yoyote? Jee twajishughulisha katika kujitayarisha kukabiliana nayo kama tunavyojitayarisha katika usafiri usioepukika au mtihani wenye kumuathiri mtu, au tumeshughulishwa mno na starehe zetu za malimwengu?

Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Enyi Mlioamini! Yasikusahaulisheni mali yenu wala watoto wenu kumkumbuka Allaah; na wafanyao hayo, hao ndio wenye kuhasirika. Na toeni katika yale tuliyokupeni, kabla mmoja wenu hayajamjia mauti, kisha akasema: 'Mola wangu! Huniakhirishi muda kidogo (tu) nikatoa sadaka na nikawa miongoni mwa watendao mema?' Lakini Allaah hataiakhirisha nafsi yoyote inapokuja ajali yake; na Allaah anazo habari za mnayoyatenda (yote)."** [Al-Munaafiqun 63:9-11].

KUNA MAPUMZIKO KATIKA MAUTI?

Pindi tunapofikwa na mauti, jee tutapata mapumziko ndani yake, au ulimwengu utapumua kwa kuondokwa kwetu? Abu Qataadah Bin Rabee' (رضي الله عنه) amepokea yakwamba palipita jeneza alipokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) siku moja, kisha akasema: *"Atapumzika au watapumzika nae."* Akaulizwa: "Wamaanisha nini kusema, *"Atapumzika au watapumzika nae."*

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

Akajibu: *"Mja aliye Mu'min atapumua na janga la dunia hii. Lakini, kwa mja muovu, basi watu, ardhi, miti na wanyama watapumua kutokamana nae."* [Imepokewa na al-Bukhaari na Muslim]

USHAJIANDAA KWA MAUTI?

Kuna baadhi ya watu hudai yakwamba ati wao wanatamani mauti na wako tayari nayo. Lakini jee, haya ni madai ya kweli. Na wanaweza kuyadumisha madai yao watakapokurubiwa na hayo mauti? Allaah (سبحانه وتعالى) amewalaumu baadhi ya watu waliopita zamani waliokuwa na madai sampuli hiyo kwa kuwaambia: **"Na nyinyi mlikuwa mkitamani mauti, kabla hamjakutana nayo. Basi mmekwisha yaona na huku mnayatazama.** [Aali 'Imraan 3:143].

Hili kwa hakika linaashiriya ukosefu wa kuwa na Imaan juu ya Allaah (kumuamini Allaah) na ahadi Zake. Mu'min wa kweli daima huwa yuko tayari kwa aina yoyote ya maonjo yawezayo kumsibu kwa ajili ya Allaah - kinyume cha wale ambao waliosifiwa na Allaah (سبحانه وتعالى) kama: **"Na katika watu wako wanaosema: 'Tumemuamini Allaah;' lakini wanapoudhiwa katika (njia ya) Allaah hufanya vile vituko vinavyowakuta kwa watu kama ni adhabu ya Allaah. Na ikija nusura kutoka kwa Mola wako husema: 'Bila shaka sisi tulikuwa pamoja nanyi.' (Na haliyakuwa ni waongo wanafiki). Jee, Allaah hajui yaliyomo vifuani mwa walimwengu?"** [al-'Ankabut 29:10]

MAVUNO MUHIMU KUTOKA KATIKA MAISHA HAYA

Basi hebu tuweni ni wakweli na waaminifu na nafsi zetu. Maisha haya si chochote, isipokuwa ni mtihani tu, basi hebu tuishini kwa 'ilmu hii, na tujivunie tunachokihitaji tu kwa ajili ya maisha yajayo. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni (kukufanyieni mtuhani); ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Naye ni mwenye nguvu na Mwenye Msamaha."** [Al-Mulk 67:2].

KUYAKUMBUKA MAUTI MARA KWA MARA

Kwahivyo, mauti yanatakiwa kuwa ni ukumbusho wetu wa daima, na kama njia ya kudhibiti mapendelewa ya nafsi zetu na kujizuiya na utapiaji. Anas na Abu Hurairah (رضي الله عنهم) wamepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Kithirisheni kuyakumbuka yenye kuangamiza starehe: mauti; kwa hakika hapana awezae kuyakumbuka anapokuwa na dhiki za kimaisha, isipokuwa ni yenye kuwakujukia; na hapana awezae kuyakumbuka anapokuwa kwenye kukunjukiwa isipokuwa yatamdhikisha maisha yake."* Mtu anapoyakumbuka mauti hudumu katika uzani wa kati na kati katika muelekeo wake wa kimaisha. Hatokwenda kwenye ncha ya kukata tamaa anapofikwa na mitihani, na wala hatokwenda kwenye ncha na kufanya kiburi na kutojali anapokunjukiwa na fadhla za kimaisha.

Zaidi ya hayo, mtu anapoyakumbuka mauti pale anapotekeleza vitendo vya Ibaada, pana uwezekano mkubwa wa kutekeleza ibaada hiyo kwa njia ya sawa. Amepokea Anas (رضي الله عنه) kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba amesema: *"Yakumbuke mauti ukiwa kwenye swala yako. Kwa hakika mtu anapoyakumbuka mauti kwenye swala yake, pana uwezekano mkubwa kwake kuitekeleza swala yake vizuri. Swali swala ya mtu ambaye hatarajii kuswali swala nyengine. Na ujiepushe na jambo lolote litakalohitaji kuomba udhuru."*

YANAYOMPASA KUFANYA ANAYEKUFA

Kadiri ya uwezo wa fahamu zake zitakavyomruhusu, anayekufa na ajaribu kuhitimisha maisha yake kwa matendo mema ambayo yatakayomdhamini kupata Pepo na kumuokoa na kila aina ya adhabu. Kila inapokuwa ni uzito kwake kudumisha uzani wa kati na kati katika matendo yake na mazungumzo yake, basi wale wenye kumuhudhuria na wajaribu kumsaidia katika jambo hilo.

FIKIRA NJEMA KUMUHUSU MOLA

Inampasa mwenye kufa kuwa na fikira njema na matumaini kumuhusu Mola wake (سبحانه وتعالى), akumbuke fadhla Zake kubwa, na atarajie Baraka Zake na Msamaha. Amepokea Jaabir Bin Abdillaah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Asife mmoja wenu bila ya kuwa na dhana njema juu ya Allaah."* [Muslim na wengineo].

BAINA YA HOFU NA MATUMAINI

Mu'min anayekufa anatakiwa aage dunia akiwa katika muungano wa hali ya hofu na matumaini: awe na hofu na adhabu ya Allaah kutokama na madhambi yake, na awe na matumaini ya kupata Rehma za Allaah.

Amepokea Anas (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amlimzuru kijana mmoja aliyekuwa katika hali ya kuaga dunia. Akamuuliza: *"Wajisikiyaje?* Akajibu: "Wallaahi, Ewe Mjumbe wa Allaah, Mimi nina matumaini na Allaah, na nina hofu juu ya madhambi yangu." Basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: *"Hazijumuiki pamoja hali mbili katika moyo wa mja aliye kwenye hali hii (ya mauti), isipokuwa Allaah (سبحانه وتعالى) humpa anayotarajia, na kumuepusha na anayohofiya."* [at-Tirmidhee na Ibn Maajah; imethibitishwa kuwa hasan na Sheikh al-Albaani].

KUPENDA KUONANA NA ALLAAH

Kila mauti yanapokurubia, mu'min wa kweli huwa na hamu kubwa sana kuonana na Mola wake (عزّ وجلّ). Hamu hii itakuwa kubwa kushinda mafungamano yoyote aliyonayo mtu na maisha au uoga wa mauti. Amepokea Shurayh Bin Haani yakwamba Abu Hurairah (رضي الله عنه) amesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Yoyote apendae kukutana na Allaah, Allaah apenda kukutana na yeye. Na yoyote anayechukia kukutana na Allaah, Allaah anachukia kukutana nae."* Basi Shurayh akenda kwa 'Aaisha (رضي الله عنها) akamwambia, "Ewe mama wa Waumini. Abu Hurairah amenisimulia hadeeth itokayo kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba, lau kama ni kweli, basi itakuwa na maana yakwamba sisi tumepotea!" Akasema ('Aaisha): "Mwenye hasara ni yule ambaye aliyethibitishwa kuwa hivyo na Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وسلم). Kwani amekusimulia nini?" Akamsimulia hiyo hadeeth, kisha akaongezea: "Hakuna yoyote miongoni mwetu isipokuwa ni mwenye kuchukia mauti!" ('Aisha) akamfafanulia maana yake: "Ni kweli yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema hivyo. Lakini haimaanishi unavyofkiria wewe! Maana yake ni kwamba, pindi macho yanapokodoka, na kifua kikaanza kunguruma (wakati roho inapotoka), ngozi hukakamaa, na vidole vikatetema - basi wakati huo ndipo, "***Yoyote apendae kukutana na Allaah, Allaah apenda kukutana na yeye. Na yoyote anayechukia kukutana na Allaah, Allaah anachukia kukutana nae."*** [al-Bukhaari na Muslim].

Mwanzoni 'Aaisha (رضي الله عنها) alikuwa ufahamu wa kimakosa kama huo ambao aliofahamishwa ipasavyo na Mtume (صلى الله عليه وسلم). 'Ubaadah Bin as-Saamit (رضي الله عنه) akaipokea

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

hadeeth hiyohiyo, akaongezea yakwamba baada ya kuisikiya kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), 'Aaisha (رضي الله عنها) akamaka, "Wamaanisha kuyachukia mauti? Sisi sote twayachukia mauti!" Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu: *"Si hivyo! Lakini pindi mauti yamjiapo mu'min, hupewa bishara njema za Rehma za Allaah, na Radhi Zake na Pepo. Hapo tena huwa hakuna akipendacho zaidi kuliko yaliyo mbele yake: Hupenda kuonana na Allaah, na Allaah anapenda kukutana nae. Lakini pindi mauti yamjiapo kafiri, hupewa bishara mbaya za hasira za Allaah, mateso na adhabu. Hapo tena huwa hakuna akichukiacho zaidi kuliko yaliyo mbele yake: Huchukia kuonana na Allaah, na Allaah anachukia kukutana nae.* [al-Bukhaari na Muslim].

KURUDISHA HAKI ZA WATU

Anaekufa anawajibika kutekeleza uwajibikaji wake kwa watu wengine kabla ya kujiliwa na mauti. Iwapo hatoweza kutekeleza hayo yeye mwenyewe, na atayarishe mipango na atoe maelekezo ya kutekeleza hayo. Abu Hurairah (رضي الله عنه) amesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Yoyote aliyemdhulumu ndugu yake kwenye hadhi yake au mali yake, basi na ayarekebishe hayo kabla ya Siku ya Malipo haijafika. Kwa sababu hakuna Dirham wala Dinaar itakayokubaliwa wakati huo: kama akiwa na Amali njema, yatachukuliwa kutoka kwake apewe ndugu yake; na kama hatokuwa na Amali njema, basi atabandikizwa na madhambi ya ndugu yake."* [al-Bukhaari na wengineo].

Vilevile Abu Hurairah (رضي الله عنه) amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliuliza: *"Nyinyi munamjua mtu aliyefilisika?"* Suali ambalo Maswahaba (رضي الله عنهم) walilolijibu: "Aliyefilisika miongoni mwetu ni yule ambaye asokuwa na pesa wala kitu chochote." Kisha akawajulisha (صلى الله عليه وسلم) yakwamba: *"Kwa hakika aliyefilisika miongoni mwa Ummah wangu nin yule ambaye atakaekuja siku ya Malipo akiwa ameswali, amefunga na ametoa Zakaa'. Lakini atakuwa amemshutumu huyu, akamtukana huyu, akachukuwa mali ya huyu kinyume cha usawa, akamwaga damu ya huyu, na akampiga huyu. Kwahiyo, hiki na kile yatalipwa kutoka kwenye amali zake njema. Iwapo amali zake njema zitamalizika kabla ya kukamilisha anayodaiwa, basi atabandikizwa madhambi yao, kisha avurumizwe ndani ya Moto."* [Muslim].

WASIYA WA MWISHO

Anayekufa na ahakikishe yakwamba wasiya wake unatumika kulingana na wakati na unafungamana na matakwa yake. Zaidi ni kwamba, anatakiwa atoe muelekeo wake wa mwisho kwa jamii yake na marafiki zake na watu wengine waliomzunguka, na awakumbushe kumuhusu Allaah, na awaelekeze wachukue tahadhari katika kutekeleza uwajibikaji wake baada ya kufa kwake. Amepokea Jaabir Bin 'Abdillaah (رضي الله عنه) yakwamba katika usiku wa kuamkia siku ya vita vya Uhud, babake alimshauri na kumuelekeza: "Mimi nataraji yakwamba nitakuwa ni miongoni mwa Maswahaba wa kwanza wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) watakaouwawa kesho. Mimi sitoacha baada yangu roho niipendayo zaidi kuliko wewe - isipokuwa kwa Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وسلم). Kuna deni ninalodaiwa, kwahivyo fanya bidii unilipie. Na uwaangalie vizuri ndugu zako wa kiume na dada zako. [al-Bukhaari].

YANAYOPASA KUFANYIWA ANAEKUFA

Pindi kifo kinapomkurubia mtu, basi wale watakaokuwa wamemuhudhuria wanawajibika kumfanyia mambo fulani kama yafuatayo:

KUMKARIRIA KUPIGA SHAHADA:

Na akazaniwe, lakini kwa utaratibu atamke Shahada (*LAA ILAA HA ILLA LLAAH Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah*). Jambo hili linaitwa *Talqeen.* Abu Sa'id al-Khudhree', Abu Hurairah, na wengineo (رضي الله عنهم) wamepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Wakaririeni wenye kufa miongoni mwenu waseme 'Laa ilaaha illallaah.' Yoyote mwenye kumaliza maneno yake wakati wa mauti yake kwa "Laa ilaaha illallaah" , basi ataingia Jannah siku moja, bila ya kujali yaliyowahi kumtokea kabla ya hapo."* [Muslim, Abu Daawud, Ibn Hibbaan na wengineo].

Amepokea Ibn Mas'ud (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *""Wakaririeni wenye kufa miongoni mwenu waseme 'Laa ilaaha illallaah.' Kwa hakika kutoweka kwa roho ya Mu'min ni (sahali) kama mfano wa kutokwa na jasho (kwa ajili ya maneno haya), haliyakuwa roho ya makafiri hutoweka kwa kupitia kwenye upande wa mdomo wake (ikiwa na harufu chafu tena yenye fujo) kama mfano wa roho ya punda."* [at-Tabaraani]

Amepokea 'Uthmaan (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Yoyote atakaekufa akiwa anajua yakwamba 'Laa ilaaha illallaah' ataingia Peponi.* [Muslim na Ahmad]

Amepokea Jaabir Bin Abdillaah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Atakaekufa haliyakuwa hakumshirikisha Allaah na kitu chochote, ataingia Peponi.* [Muslim na Ahmad].

Kukariri huko hakufanywi kwa kujisemea tu Shahada hiyo kwenye hadhara ya anaekufa ili apate kuisikia. Bali anatakiwa kuamrishwa na kusaidiwa ili aitamke yeye mwenyewe. Anas (رضي الله عنه) amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimzuru mtu aliyekuwa kwenye mauti ma-Answaar wakasema kumwambia: "Ewe Mjomba! sema, "*LAA ILAAHA ILLA LLAAH."* Akauliza, kwani mimi ni mjombako kwa upande wa Baba au upande wa mama?" akajibu, "Kwa upande wa mama." Akamuuliza, "Ni jambo zuri kwangu mimi kusema, 'LAA ILAAHA ILLA LLAAH.'" Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu: *"Na'am."*

Ni jambo la wazi kutokamana na hadeeth hii yakwamba huyu mtu alikuwa akipotewa na fahamu zake, na alikuwa zaidi akitaka kujua uhusiano wake na Mtume (صلى الله عليه وسلم) hata kuliko kupiga shahada. Juu ya hayo yote, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa na bidii kumtamsha Shahada, na katika hali hiyo akawa ni mwenye kumjibu masuali yake mengine.

KUOMBA DU'AA NA KUTAMKA MANENO MAZURI

Wakati wa kumtembelea mtu aliyekurubia kufa, anatakiwa mtu amuombee Du'aa na atamke maneno mazuri yenye kumuashiriya bishara njema. Amepokea Umm Salamah (رضي الله عنها) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Utakapokuwa pamoja na mgonjwa au mtu aliyekurubia kufa, sema maneno yaliyo mazuri, kwa sababu Malaika huitikia unayoyatamka (kwa kuitikia Aameen.)"* . Umm Salamah (رضي الله عنها) akaongezea yakwamba alipokufa Abu Salamah (رضي الله عنه), alikwenda kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akamwambia, "Yaa Rasoolullaah! Abu Salamah ameaga dunia." Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamuamrisha aseme: *"Yaa Allaah nisamehe mimi na yeye, na unipe badala yake kwa kilicho kizuri."* Akamalizia , "Kisha Allaah akanipa badala yake aliyekuwa ni bora kwangu mimi kuliko yeye: Muhammad (صلى الله عليه وسلم)!" [Muslim, Baihaqee].

UMUHIMU WA SUNNAH

Na: QSSEA

[ENDELEA KUTOKA VOL14 / ISSUE 1]

Siku moja 'Abdullaah ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) alikuwa amekaa karibu na Al-Ka'bah, mara akamuona Ameer Mu'aawiyah (رضي الله عنه) akiingia katika Msikiti Mtukufu na akaanza kutufu al-Ka'bah, mwanzo akalibusu jiwe jeusi, lakini akazipangusa pembe tatu za Ka'bah kwa mikono yake (yaani; Syra, Iraq na Yemen). Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) alikuwa yuwajua yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) mbali na kulibusu jiwe jeusi na kupangusa mikono yake katika pembe ya Yemen – hakuwahi kuzigusa pembe nyengine wakati wa tawaf. Kwahivyo alimkataza Mu'awiyah, naye akajibu: 'Mimi siachi pembe yoyote ya Ka'bah.'' Ibn 'Abbaas akasisitiza, 'Lakini hayo si mafundisho ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). Baada ya kuyasikiya hayo, jawabu la Mu'aawiyah (رضي الله عنه) halikuwa jengine isipokuwa: 'Maneno yako ni ya kweli.'

Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) alimuona mtu akichora picha ya kiumbe mwenye uhai. Akamuonya awachane na shughuli hiyo kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitukataza kufanya jambo hilo. 'Abdullaah ibn 'Umar (رضي الله عنه) alikuwa akijulikana mno kwa kujiambatanisha na Sunnah. Siku moja alimuona mwanae Bilaal akimzuiya mkewe asende msikitini. 'Abdullaah ibn 'Umar (رضي الله عنه) akasema, "Usifanye hivyo kwa sababu Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Musiwazuiye waja wa kike wa Allaah kuingia katika nyumba ya Allaah." Bilaal akashika kani yakwamba hatomruhusu kattu hata baada ya kuyasikiya hayo maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). Jambo hilo likamkasirisha sana Ibn 'Umar (رضي الله عنه) mpaka akala kiapo yakwamba hatozungumza tena na mwanae huyo hadi siku yake ya kufa.

'Abdullaah ibn 'Amr ibn al-'Aas alikuwa na bustani kubwa lilokuwa na idadi nyingi sana ya michikichi (Palm-trees). Mahali hapo palikuwa na maji mengi mno hata ikambidi msaidizi wake afanye mipango ya kumuuzia jirani yake kiwango cha ziada (cha maji hayo) baada ya kumaliza mradi wa umwagiliaji kwenye bustani lake. Dirham elfu thalathini ndicho kiwango walichoafikiana, nayo ilikuwa ni bei kubwa kupita kiasi. Hiyo ni bei itakayomvutia mtu yoyote kwa wakati huo isipokuwa Swahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) 'Abdullah ibn 'Amr aliyekataa kuikubali bei hiyo kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikataa kuuza maji yoyote ya ziada.

Abu Huraira alikuwa akiwatolea darsa Waislamu katika usiku wa Alkhamisi (Ijumaa usiku). Siku moja, kabla ya kuanza darsa yake alitangaza kwa watu: 'Mtu yoyote miongoni mwenu hapa aliyejitenga na kujiepusha na kizazi chake na aondoke mahali hapa.' Hapana mtu yoyote kwenye kongamano hilo aliyeondoka. Baada ya kuyakariri maneno hayo kwa mara tatu, kijana mmoja akainuka mahali hapo na akaondoka kuelekea moja kwa moja hadi kwa shangazi yake, ambae aliyemuhama kwa muda mrefu, na akarudisha uhusiano nae. Abu Huraira aliyasema hayo kwa sababu alikuwa akijua yakwamba matendo yote hudhihirishwa kwa Allaah kila ifikapo usiku wa Ijumaa. Abu Huraira hakupendezwa kongamano hilo la wacha Mungu litiwe doa na mtu aliye na dhambi za kuwakata jamaa zake. Kwa kufanya hivyo, alimuokoa mtu kutokana na madhambi makubwa.

Anas bin Maalik (رضي الله عنه) alijulikana kama mtumishi muaminifu wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Siku moja alialikwa kwenye karamu ambapo Mmajusi alimkaribisha ale *FALUDA* (aina ya kinywaji maarufu) kwenye kikombe cha fedha nae Anas (رضي الله عنه) akakataa kupokea. Alikhiyari kunywa kwenye kijungu cha udongo kuliko kutumia chombo cha fedha kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitukataza Waislamu tusile wala tusinywe kwenye vyombo vya dhahabu au fedha.Hii ndiyo mifumo waliyokuwa nayo Maswahaba waheshimiwa katika maisha yao wakiwa ni vielelezo kwetu jinsi ya kujilazimisha na kujiambatanisha na Sunnah za Bwana Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Mifano hiyo chungu nzima iliyopita ni kutoka kwa Maswahaba (رضوان الله عليهم). Hebu sasa tuangalieni yale waliyoyasema Maimamu wanne watukufu kuhusu mamlaka ya Sunnah.

Imaam Abu Hnaneefah (رحمه الله): "Tufanyeje sisi iwapo tutakuta yakwamba maneno yako yanakwenda kinyume na Kitabu cha Allaah?" Nae akajibu, "Wachaneni na maneno yangu na mushikamane na Kitabu cha Allaah." Muulizaji akauliza, "Jee iwapo maneno yako yatakhitilafiana na maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)?" Akasema, "Yaacheni maneno yangu kwenye uso wa maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)." Akaendelea kuulizaa muulizaji, "Jee iwapo maneno yako yatakwenda kinyume na maneno ya Swahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم)?" Akajibu tena, "Yaacheni maneno yangu kwenye uso wa maneno ya Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم)." [Al-Qawl al-Mufeed cha Imaam ash-Shawkaani].

Imaam Abu Hanifah pia alieleza waziwazi yakwamba, 'Njia yangu (madh-hab) ni chochote kilichopasishwa na hadeeth iliyo saheeh.' [Shami 1:50, al-Fulani katika "Iqaz" uk.62].

b) Maneno ya *Imaam Maalik bin Anas* (رحمه الله) ni maarufu sana, "Maneno ya kila mmoja yanaweza kukubaliwa au kukataliwa, isipokuwa kwa Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم)." [Ibn 'Abdul Barr, ibn Hazim, pia katika al-Yawaqeet wal Jawahir 2:96].

Pia akasema, "Mimi si chochote zaidi ya mwana-adamu tu; wakati fulani hukosea, na wakati fulani hupata. Kwahivyo kuweni waangalifu katika raiy zangu: chochote chenye kukubaliana na Kitabu na Sunnah, kikubalini, na chochote chenye kukhitilafiana na Kitabu na Sunnah, kiwachilieni mbali." [al-Fulani katika "Iqaz" uk.72].

c) Siku moja *Imaam ash-Shaafi'i* (رحمه الله) alipokea Hadeeth, mtu fulani katika waliohudhuria kikao chake akasema, "Na wewe pia waafikiana na hiyo (hadeeth)?" Aliposikia maneno hayo, Imaam ash-Shaafi'i alikasirika sana. Uso wake ulibadilika rangi na kukwajuka (pale) na akasema, "Ole wako! Ni ardhi gani hiyo itakayonihimili mimi, na ni mbingu gani zitakazonihifadhi mimi, ikiwa nitapokea hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kisha niwe na raiy tafauti! Kwani umeniona na Zunnar (aina ya ukanda unaovaliwa na makafiri) mwilini mwangu? Au uliniona mimi nikitoka kanisani? Itakuwaje mimi nipokee hadeeth kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na nisikubaliane nayo?!"

d) *Imaam Ahmad ibn Hanbal* (رحمه الله) amesema, "Usinifuate mimi wala Maalik, wala Shaafi'i, wala Auza'i, wala Thauri, lakini chukuwa kutoka pale walipochukuwa wao (yaani kutoka katika Qur'aan na Sunnah zilizo Saheeh)." [al-Fulani, ibn al-Qayyim] Vilevile alisema, "Yoyote mwenye kuyakanusha maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) yuko kwenye ukingo wa maangamivu." [ibn al-Jauzi].

NENO LA BUSARA

Imaam Maalik Bin Anas (رحمه الله): "Maneno ya kila mmoja wetu, isipokuwa mwenye kaburi hili [Mtume (صلى الله عليه وسلم)], yanaweza kukubaliwa au kukataliwa."